Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 8, Issue 3, 2025
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

Masuala Ibuka Yanayowasilishwa katika Vikatuni vya Ubongo Kids

Stephen Odiwuor Opondo[1], Dkt. Mary Kanyua, PhD[1] na Dkt. Onesmus Ntiba, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S.L.P 109, Chuka, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: odiwuor813@gmail.com

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Tarehe ya Uchapishaji:

11 Novemba 2025

Istilahi Muhimu:

Vikatuni, Ubongo Kids, Masuala ibuka, Elimu ya kidijitali, Uendelevu wa mazingira.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kujadili masuala ibuka kwenye vikatuni vya Ubongo Kids. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Elimu Burudani ambayo iliwekewa msingi na Miguel Sabido (2003). Elimu Burudani ni nadharia iliyofumwa kuelimisha na kubadilisha mitazamo ya jamii kupitia burudani. Nadharia ya Elimu Burudani ilimsaidia mtafiti kuelewa jinsi vikatuni vya Ubongo Kids vinavyoelezea hali halisi kuhusu maisha ya watu na jinsi watazamaji wanaweza kuchochewa kujenga maana fulani kwa kulinganisha matukio katika kipindi na maisha yao. Sampuli ya utafiti ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji kimaksudi. Mbinu ya usampulishaji kimaksudi ilimhitaji mtafiti kuamua kwa hiari yake sampuli iliyoweza kumpa data kutoka kwa video inayohusiana na lengo la utafiti. Ukusanyaji wa data ulitumia mbinu ya kiwango kifu ambapo hakuna masuala au maarifa mapya yaliyobainika na data ilianza kujirudia, jambo linaloashiria kuwa ukubwa wa sampuli uliokusudiwa umefikiwa. Hivyo, mtafiti aliteua video 10. Uteuzi wa video ulizingatia masuala ibuka, ubora wa elimu kupitia burudani, na uhusiano wa moja kwa moja na malengo ya utafiti. Pia, video zilichaguliwa kulingana na ubora wa kiufundi na kipindi cha ubunifu kati ya mwaka wa 2014 na 2025. Data ilikusanywa kwa kutazama kauli na matendo yaliyoashiria masuala ibuka na kauli yao kunukuliwa. Uchanganuzi pamoja na uwasilishaji wa data ulifanyika kwa njia ya maelezo. Utafiti ulibaini kuwa masuala ibuka katika vikatuui vya Ubongo Kids huwasilishwa kwa njia rahisi kueleweka, yakilenga kuelimisha watoto kuhusu changamoto za sasa kama mabadiliko ya tabianchi, ulinzi wa watoto, matumizi salama ya teknolojia, umuhimu wa lishe bora, elimu na usafi wa mazingira. Matokeo ya utafiti yatawafaidi walimu, wakuza mitalaa na watafiti wengine kwa kuonyesha ufaafu wa vipindi vya watoto kama kiungo muhimu cha elimu kando na kuburudisha.

APA CITATION

Opondo, S. O., Kanyua, M. & Ntiba, O. (2025). Masuala Ibuka Yanayowasilishwa katika Vikatuni vya Ubongo Kids. *East African Journal of Swahili Studies*, *8*(3), 15-32. https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

CHICAGO CITATION
Opondo, Stephen Odiwuor, Mary Kanyua and Onesmus Ntiba. 2025. "Masuala Ibuka Yanayowasilishwa katika Vikatuni vya Ubongo Kids". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (3), 15-32. https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

HARVARD CITATION
Opondo, S. O., Kanyua, M. & Ntiba, O. (2025) "Masuala Ibuka Yanayowasilishwa katika Vikatuni vya Ubongo Kids", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(3), pp. 15-32. doi: 10.37284/jammk.8.2.3948

IEEE CITATION
S. O., Opondo, M., Kanyua & O., Ntiba "Masuala Ibuka Yanayowasilishwa katika Vikatuni vya Ubongo Kids", *EAJSS*, vol. 8, no. 3, pp. 15-32, Nov. 2025.

MLA CITATION
Opondo, Stephen Odiwuor, Mary Kanyua & Onesmus Ntiba "Masuala Ibuka Yanayowasilishwa katika Vikatuni vya Ubongo Kids". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 3, Nov. 2025, pp. 15-32, doi:10.37284/jammk.8.3.3948.

UTANGULIZI

Vipindi vya watoto duniani vimepitia mageuzi makubwa tangu kuanzishwa kwa Nickelodeon mwaka 1979, kituo kilichojitolea kurusha vipindi kwa kuzingatia umri wa watoto (Imaizumi, 2009). Mafanikio yake yalipelekea kuibuka kwa vituo vingine kama Cartoon Network na Disney Channel, ambavyo vilienea duniani kote kufikia miaka ya 1990. Nchini Kenya, historia ya vikatuni ilianza miaka ya 1950 kupitia magazeti, kisha ikaendelea na upanuzi wa vyombo vya habari na majukwaa ya kidijitali katika miaka ya 1990 hadi sasa (Callus, 2018; Karani, 2021). Kuongezeka kwa utazamaji wa televisheni na mtandao, pamoja na umaarufu wa vikatuni, kumeongeza nafasi ya vyombo vya habari katika kuelimisha na kuburudisha watoto.

Katika muktadha wa Kenya, vipindi vya watoto kama *Ubongo Kids* vimepata umaarufu kwa kutumia njia ya burudani kufundisha masomo kama sayansi, hisabati, na stadi za maisha. Gitonga (2020) anasema kuwa idadi wastani ya watazamaji wa televisheni chini ya miaka kumi na minne nchini Kenya siku yoyote ile ni milioni moja na elfu mia mbili. Idadi hii inapatikana kati ya saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni.

Ubongo Kids ni vipindi vya vikatuni vinavyobuniwa Tanzania na ni maarufu barani Afrika kutokana na mbinu yake ya kipekee ya kufundisha watoto (Ubongo, 2024). Vipindi hivi vimechochea hamu nchini Kenya kutokana na thamani yao ya kielimu na maudhui yanayohusiana na changamoto zinazokumba jamii za Kiafrika na ulimwengu. Vikatuni sasa vinaakisi masuala ibuka kama vile afya na mazingira, hivyo kuchochea hoja ya ujumuishaji wa maudhui haya katika mitaala ya shule na fasihi ya watoto (Wizara ya Elimu, 2002). Watafiti mbalimbali kama vile Prithviraj na wenzake (2024), Boyd (2015) na Neil (2012) wanaonyesha kuwa vikatuni vina nguvu ya kuathiri mitazamo ya kijamii, na vinaweza kutumiwa kama lugha ya picha yenye ufanisi wa kuwasilisha ujumbe. Kwa hivyo, mtafiti alichochewa kuchunguza mchango wa vikatuni kama *Ubongo Kids* katika kukuza uelewa wa masuala ibuka miongoni mwa watoto nchini Kenya.

Suala la Utafiti

Vikatuni ni mojawapo ya zana maarufu ambazo huburudisha watoto kando na kuwa na uwezo wa kutumika kama nyenzo ya kuunda, kubadilisha na kuathiri mitazamo ya watoto. Nchini Kenya, watoto hutumia muda mwingi kutazama vipindi wapendavyo kwenye televisheni. Matumizi ya burudani kupitisha ujumbe wa kielimu kupitia vyombo vya habari pia umepata umaarufu. Hata hivyo, mabadiliko ya haraka katika mazingira ya vyombo vya habari, pamoja na changamoto zinazoibuka katika jamii inasababisha kuwepo kwa haja ya kuchunguza ikiwa yapo mambo yanayoathiri jamii ya kisasa kwenye vipindi hivi ili kueleweka kwa kina. Pia, ipo haja ya kukuza watoto tangu utotoni mwao kuhusiana na mambo yanayoathiri jamii. Ingawa vipindi vya *Ubongo*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Kids vimefanikiwa kuwavutia watoto, kuna haja ya kuchunguza vipindi hivi kutokana na mabadiliko ya mahitaji ya kielimu na kijamii. Kwa hivyo, utafiti huu ulinuia kuchunguza uwasilishaji wa masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*.

YALIYOANDIKWA KUHUSU MASUALA IBUKA

Masuala ibuka, kama yalivyoelezwa na Maureen (2015) na Simala (2016), ni mabadiliko mapya yanayoathiri jamii ya kisasa katika nyanja mbalimbali kama vile siasa, uchumi, teknolojia, dini na jamii. Simala anaongeza kuwa masuala haya yanaweza kuwa mambo yaliyokuwepo lakini yameanza kuchukuliwa kwa uzito mpya, au ni masuala ambayo awali hayakuzingatiwa sana lakini sasa yanaonekana kuwa na umuhimu. Jamii za sasa hukumbwa na changamoto kama dawa za kulevya, dhuluma dhidi ya watoto, ufisadi, uongozi mbaya na masuala ya kijinsia. Haya yote yanahitaji kushughulikiwa kwa njia za ubunifu na zinazofaa umri wa walengwa, hasa watoto.

Katika muktadha wa vyombo vya habari, Kidenda (2006) anaeleza kuwa vikatuni vina ushawishi mkubwa kwa watoto kwa kuwa vinawasilisha utamaduni na mitazamo ya kijinsia. Ingawa baadhi ya vipindi vinaendeleza dhana zilizopitwa na wakati kuhusu nafasi za wanaume na wanawake, utafiti huu unaonyesha kuwa vikatuni vinaweza pia kutumika kwa njia chanya kuelimisha watoto kuhusu masuala ibuka ya kijamii na kimazingira. Hii ni kinyume na mitazamo ya awali iliyodhani vikatuni ni burudani tu bila mchango wa kielimu. Tofauti na utafiti wa Kidenda (keshatajwa), utafiti huu ulibaini kuwa vipindi vya vikatuni vina uwezo wa kutumika kama chombo chanya ya kuburudisha na kuelimisha kuhusu changamoto za kijamii na kimazingira.

Eko (2010) anaeleza kuwa tangu mwanzo mwa miaka ya 1990, vikatuni vimeongoza mapambano ya uhuru wa kujieleza Barani Afrika. Uchambuzi wa sampuli za kimakusudi za vikatuni kutoka nchi ambazo zimekuwa na mapambano makubwa kati ya serikali na vyombo vya habari ulibaini kwamba vikatuni vya kisiasa vya Kiafrika husheheni mazungumzo ya upinzani yasiyo na heshima. Pia vikatuni hivi hutumia semi na hadithi za Kiafrika kuonyesha taswira ya huzuni kuhusu hali ya vyombo vya habari barani Afrika. Aidha, mbinu moja ambayo vikatuni vya Kiafrika vimetumia kukemea uongozi wa kimabavu ni kwa kuangazia ukandamizaji wa kisiasa dhidi ya vyombo vya habari. Wanaobuni vikatuni wako mstari wa mbele katika upinzani dhidi ya matumizi mabaya ya madaraka na ukiukaji wa haki za binadamu barani Afrika. Ingawa Eko (keshatajwa) anatoa uchambuzi wa kina kuhusu vyombo vya habari vya Afrika kupitia vikatuni vya kisiasa, mchango wake katika masuala ibuka ni mdogo, pengo lililozibwa na utafiti huu.

Vilevile, watafiti kama Nanda (2011) na Maureen (2015) wameangazia umuhimu wa kuhifadhi mazingira na changamoto za kijamii katika kazi za kifasihi. Nanda anaangazia dhima ya binadamu katika uharibifu wa mazingira na umuhimu wa kuwajibika, lakini hakueleza jinsi fikra hizo zinaweza kuwafikia watoto. Maureen naye anaangazia riwaya za watu wazima ambazo huchambua masuala ibuka kwa mtazamo mzito, lakini utafiti huu unaonyesha kuwa vikatuni ni njia mwafaka zaidi ya kufikisha ujumbe huo kwa watoto kwa kutumia mbinu kama elimu burudani na usimulizi wa kuvutia.

Motswaledi (2022) alichunguza jinsi vikatuni vinatumika kama chombo chenye uwezo wa kufikisha suala tata la mabadiliko ya hali ya hewa. Vikatuni hurahisisha mada hii kwa kuonyesha matatizo ya kimazingira kama vile uchafuzi wa mazingira, ukataji miti, na hali mbaya ya hewa kwa njia inayovutia na kueleweka. Kinyume na vikatuni vya kawaida, vikatuni vya kisiasa vina jukumu muhimu si tu la kudhihaki na kuchekesha bali pia kubeba taarifa kwa njia ya ucheshi na busara. Zaidi ya hayo, uwezo wa vikatuni wa kuhifadhi na kuendeleza masuala katika jamii umekuwa muhimu katika kuharakisha uelewa juu ya uharibifu wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa njia hii, ni wazi kwamba vikatuni vya kisiasa vinaunda sehemu muhimu ya vyombo vya habari vinavyotoa taarifa, kuhifadhi, na kuangazia maovu ya kijamii. Utafiti wa Motswaledi ulionyesha jinsi vikatuni viliweza kurahisisha masuala magumu kama mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutumia picha zenye mvuto na ujumbe rahisi kueleweka. Motswaledi (2022) alifanya utafiti kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa ambayo ni suala ibuka bali utafiti huu uliangazia masuala ibuka kwa jumla kama vile elimu ya kidijitali, ulinzi wa watoto pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Watafiti wengine kama Ngugi (2017), Opunde na wenzake (2018) na Wesonga na wenzake (2020) wametoa michango tofauti kuhusu jinsi fasihi, muziki, na vyombo vya habari vinavyoangazia masuala ibuka. Ngugi (keshatajwa) alisisitiza nafasi ya hadithi kwa watoto, huku Opunde na wenzake wakieleza picha za kijinsia katika nyimbo. Utafiti huu unazidi kuonyesha kuwa vikatuni vinaweza kuwa daraja kati ya elimu ya watu wazima na watoto, kwa kuwasilisha maudhui mazito kwa njia rahisi, ya kuvutia na yenye kuelimisha, ambayo watoto wanaweza kuelewa na kuhusiana nayo.

Hatimaye, Ikoro (2022) alitafiti kuhusu vikatuni kama chombo halisi cha mabadiliko katika jamii. Mtafiti alijikita katika sampuli ishirini za vikatuni kuanzia Agosti 1 hadi 11, 2021, kule Nigeria. Utafiti ulibaini kuwa wanaobuni vikatuni huvitumia kutoa maoni kwa siri juu ya masuala ya sasa kwa njia ya kejeli ambayo inaweka wazi maovu ya kijamii kwa lengo la kuyarekebisha. Wanaobuni vikatuni huonyesha uzito wa mzigo ambao unatokana na maovu katika jamii kama vile ufisadi kwa taifa ya Nigeria. Vikatuni vina jukumu juu ya maoni ya umma kwa kupunguza ugumu wa kuelewa mambo ya kijamii ili kuleta mabadiliko, pale panapohitajika. Aidha, katika jamii yenye kiwango kikubwa cha watu wasio na elimu, vikatuni vinaweza kufanikisha mawasiliano kwani vikatuni hueleweka kwa urahisi kwa wale wenye elimu ya kiwango cha chini. Kwa kuwa vikatuni hupendwa na watoto, Ikoro alidhihirisha kuwa dunia inabadilika haraka na watoto wanahitaji njia ya kuelewa mabadiliko hayo. Hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa elimu burudani huweza kufanikisha masuala ibuka kwa watoto ili waweze kukuzwa tangu utotoni mwao kuhusu masuala haya. Vikatuni vinakidhi mahitaji haya kwa uwezo wao wa kubadilika ili kuakisi hali halisi katika jamii.

Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Elimu Burudani. Nadharia ya Elimu Burudani uhusisha matumizi ya burudani kama njia ya kuelimisha na kushawishi hadhira kwa kuwasilisha maudhui ya kijamii kupitia hadithi na wahusika wanaohusiana na mazingira ya watazamaji (Sharma, 2023). Nadharia hii, iliyobuniwa na Miguel Sabido, inategemea msingi wa nadharia ya Utambuzi wa Kijamii ya Bandura, ambapo watu hujifunza kupitia kuangalia tabia za wengine na matokeo yake (Sabido, 2003). Vipengele muhimu vya nadharia hii ni pamoja na matumizi ya muziki, filamu, na michezo; ushirikiano wa vyombo vya habari na mawakala wa mabadiliko, pamoja na kuwasilisha ujumbe wa elimu ndani ya burudani bila kuathiri mvuto wa simulizi. Nadharia ya Elimu Burudani inahimiza wasikilizaji au watazamaji kufikiri kwa undani juu ya masuala yaliyowasilishwa, na kusababisha uelewa bora. Isitoshe, kuwatazama wahusika wakifanikiwa kutokana na masuala fulani yanayowakumba huongeza imani ya watazamaji katika uwezo wao wa kufikia matokeo sawa. Hata hivyo, ujumbe wa elimu huunganishwa katika maudhui ya burudani bila kuathiri kipengele chochote. Kwa kutumia vipengele hivi, Elimu Burudani inalenga kuunda maudhui ya kuvutia watazamaji kando na kukuza mabadiliko mazuri ya kijamii na tabia (Brown, 2017). Kwa msingi huu, utafiti ulichunguza vipindi vya *Ubongo Kids* na kubaini jinsi vinavyotumia burudani kufanikisha ufundishaji wa masuala ibuka kwa watoto. Kupitia elimu burudani, watazamaji huhimizwa kutafakari, kushiriki na kubadilisha tabia katika jamii (Sabido, 2003).

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo uliomwezesha mtafiti kukusanya na kuchambua data kwa njia ya kina na wazi (Orodho, 2003). Eneo la utafiti lilikuwa mtandao wa *YouTube*, ambapo vipindi vya *Ubongo Kids* vilipatikana ili kufanikisha uchunguzi na urejeleo wa matukio. Uteuzi wa sampuli ulifanywa kimaksudi. Vigezo vilivyotumika kuchagua video kwa ajili ya uchambuzi vililenga kupata data sahihi. Kwanza, video zililazimika kuzingatia masuala ibuka. Pili, video zilihakikisha kutoa elimu kwa njia ya burudani. Tatu, ujumbe wa kila video ulipaswa kulingana moja kwa moja na malengo makuu ya utafiti. Mwisho, vigezo vya muda na ubora wa kiufundi vilizingatiwa. Video zilipaswa kuwa zimebuniwa kati ya 2014 na 2025. Data zilikusanywa kwa kutazama video na kutumia orodha ya ukaguzi ili kunukuu matukio, kauli na tabia za wahusika kwa lengo la kuchanganua masuala ibuka. Mbinu ya kiwango kifu ilitumika ili kuhakikisha kuwa sampuli iliyochaguliwa ilikuwa tosha na ya kina (Naeem na wenzake, 2024). Uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kupanga vipengele katika makundi matatu: masuala ibuka, mbinu za uwasilishaji, na usawiri wa wahusika, kwa mwongozo wa nadharia ya Elimu Burudani. Hatimaye, matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo, kwa kutumia nukuu na mifano kutoka vipindi husika ili kuonyesha jinsi maudhui ya elimu yalivyofanikishwa kupitia burudani.

MATOKEO NA MAJADILIANO

Masuala Ibuka Katika Vipindi Vya *Ubongo Kids*

Sehemu hii inaangazia matokeo kuhusu masuala ibuka katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids.*

Mabadiliko ya Tabianchi

Kwa mujibu wa *Intergovernmental Panel on Climatic Change* (*IPCC*) (2013), mazingira ya binadamu yako katika hatari ya kuangamia kutokana na mienendo ya binadamu. Mienendo hii inajumuisha ukataji wa miti, ujenzi wa kiholela katika maeneo ya mabondeni, matumizi ya teknolojia yenye madhara kwa mazingira na ukosefu wa uadilifu katika uongozi. Matokeo ya vitendo hivi ni ongezeko la joto duniani, mabadiliko mabaya ya hali ya hewa, kuenea kwa magonjwa, vifo, kupungua kwa mavuno, na hatimaye kuongezeka kwa njaa. Sehemu hii inaangazia chanzo cha mabadiliko ya tabianchi, madhara ya mabadiliko ya tabianchi na jinsi madhara haya yanaweza kuepukwa kulingana na vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*.

Chanzo cha Mabadiliko ya Tabianchi

Kama anavyosema Vasquez (1983), fasihi ina mchango mkubwa katika kuendeleza maadili na kuunda mitazamo ya wanadamu kuhusu masuala mbalimbali katika jamii. Kadri mazingira yanavyoendelea kubadilika, ndivyo fasihi inavyozidi kuchukua jukumu la kuchunguza hali ya jamii, kwa kutumia mbinu mpya za uandishi, mitazamo ya kina ya kimajadiliano, na kushughulikia matatizo yanayoibuka katika jamii ya kisasa. Ndani ya kazi hizi za kifasihi, maudhui hutumika kuakisi uhalisia wa maisha ya kijamii (Wesonga na wenzake (2020). Kwa kuwa suala la mazingira ni suala la kijamii, linapaswa kuchunguzwa kwa kina, hasa linapojitokeza katika fasihi, kwa kuwa huwa linaonyesha mitazamo na hisia za wanajamii.

Mabadiliko ya tabianchi husababishwa na shughuli mbalimbali katika jamii katika vipindi vya *Ubongo Kids*. Kwa mfano:

Koba: …Lakini pia sisi tunhitaji utusaidie, tunataka kujifunza kuhusu mabadiliko ya tabianchi na dharura ya tabianchi

Baraka: Ili tumshawishi Shiko kuja kujenga kituo cha kuzalisha umeme hapa Kokotoa

Koba: Na hili litasaidia marafiki zake Nina waliopoteza shule yao kwenye mafuriko...

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Kibena: Nafikiri ninajua kinachosababisha mabadiliko ya tabianchi… Ninachokumbuka ni kwamba, tukichoma mafuta kwenye gari au pikipiki au kuchoma mkaa kwa ajili ya kupikia au kuchoma takataka, tunatoa hewa ya kabonidioksaidi angani. Kabonidioksaidi ni hewa ukaa.

Koba: Hewa ukaa hairuhusu joto kutoka kwenye dunia…

(Ubongo Kids Kiswahili 2021a, 0:33 - 1:21)

Kwa mujibu wa dondoo hili, chanzo kikuu cha mabadiliko ya tabianchi ni shughuli za binadamu kama vile kuchoma mafuta kwenye magari na pikipiki, kuchoma mkaa kwa kupikia, na kuchoma takataka. Shughuli hizi hutoa hewa ya kabonidioksaidi (hewa ukaa) ambayo inapojikusanya angani hairuhusu joto kutoka duniani hivyo kuvuruga hali ya hewa ya kawaida. Hali hii husababisha athari kama mafuriko ambayo yanaafikiana na mawazo ya Greg (2004) anayeeleza kuwa matatizo ya mazingira yanaweza kufikishwa kwa jamii kupitia fasihi, kwani fasihi ina uhusiano wa karibu sana na utamaduni wa jamii. Kwa mujibu wa Sabido (2003), kutumia burudani kama njia ya mawasiliano husaidia kuelimisha watoto na vijana kuhusu sababu hizi kwa namna rahisi na ya kuvutia. Hali hii huwezesha watazamaji kuelewa athari za matendo yao kwa mazingira na kuwahamasisha kubadili tabia zao ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Madhara ya Mabadiliko ya Tabianchi

Mabadiliko ya tabianchi ni tatizo la kimataifa linalozidi kushika kasi kutokana na ongezeko la shughuli za binadamu zinazoathiri mazingira. Madhara ya mabadiliko ya tabianchi yameanza kuonekana wazi katika sehemu mbalimbali za dunia, yakileta changamoto katika maisha ya binadamu, viumbe hai na mifumo ya ikolojia. Ifuatayo ni baadhi ya madhara makuu ya mabadiliko ya tabianchi kulingana na vipindi husika katika vikatuni vya *Ubongo Kids*.

Ongezeko la Joto Ulimwenguni

Njeru na wenzake (2022) wanaeleza kuwa mazingira asilia kama vile misitu, mito, milima na maziwa ni sehemu muhimu katika maisha ya binadamu kwani yanatoa mahitaji ya msingi kama chakula, maji, hewa safi na makazi. Hata hivyo, kutokana na kuongezeka kwa viwango vya joto duniani na mabadiliko ya tabianchi, kumekuwa na wasiwasi mkubwa katika jamii ya kimataifa. Hali hii imeibua mijadala ya kitaifa na kimataifa kuhusu namna bora ya kuhifadhi mazingira, kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali asilia. Kwa hivyo, mjadala huu umechochewa na uelewa wa kwamba mazingira ni rasilimali na nguzo kuu ya maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Suala la ongezeko la joto katika eneo la Kokotoa kwenye kipindi cha *Ubongo Kids* inadhihirika katika mazungumzo kati ya Nina na Koba:

Nina: Aise! Nahisi naweza kuyeyuka hapa! Hivi kokotoa ndio huwa kuna joto namna hii?

Koba: Huwa kuna joto lakini sio kama hili

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 17:09- 17:19)

Katika mazungumzo kati ya Nina na Koba, kuna ongezeko la joto lisilo la kawaida katika eneo la Kokotoa. Nina anaeleza kuwa anahisi kama anaweza kuyeyuka kutokana na joto kali, jambo linaloonyesha mshangao na wasiwasi wake kuhusu mabadiliko yasiyo ya kawaida katika hali ya hewa. Koba anasisitiza kuwa Kokotoa huwa na joto, lakini anasisitiza kuwa kiwango cha joto cha sasa si cha kawaida. Mazungumzo haya yanaangazia athari za mabadiliko ya tabianchi, hasa kuongezeka kwa mawimbi ya joto kali ambayo huathiri mifumo ya ikolojia na afya ya binadamu. Suala la ongezeko la joto linawasilishwa kupitia burudani ili kuvutia watoto ili kuafikiana na mawazo ya Sharma (2023) kuwa burudani inaweza kutumika kama chombo cha kuelimisha na kushawishi tabia chanya katika jamii. Kupitia burudani, kipindi hiki cha *Ubongo*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Kids huchochea uelewa wa kijamii kuhusu ongezeko la joto na umuhimu wa kulinda mazingira.

Kukosekana kwa Vyakula

Toromade na wenzake (2024) wanaweka wazi kuwa mabadiliko ya tabianchi yanawasilisha vikwazo vikubwa kwa uwepo wa chakula duniani, kwa kuvuruga uzalishaji wa kilimo, kuongeza uhaba wa chakula, na kuzidisha utapiamlo. Mabadiliko ya halijoto na mifumo ya mvua, pamoja na kuongezeka kwa matukio ya hali mbaya ya hewa, yanatishia mazao ya kilimo, afya ya mifugo na mifumo ya usambazaji wa chakula hasa katika maeneo yaliyo hatarini.

Katika vipindi vya *Ubongo Kids*, mabadiliko ya tabianchi ina madhara kwenye sekta ya ukulima. Haya yanadhihirika wazi kutokana na mazungumzo kati ya Baraka na Mama:

Baraka: Shikamoo, tunatafuta maparachichi

Mama: Poleni wanangu, sijapata maparachichi zaidi ya wiki sasa.

Baraka: Jameni! Hata sokoni hatukupata hata moja

Mama: Ni kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Hakuna maji ya kutosha kwa ajili ya maparachichi.

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 19:33- 19:49)

Mazungumzo haya kati ya Baraka na Mama yanadhihirisha jinsi mabadiliko ya tabianchi huathiri maisha ya kila siku ya watu, hasa katika sekta ya kilimo na upatikanaji wa chakula. Baraka na mwenzake wanaonekana kutafuta maparachichi bila mafanikio. Mama anawaeleza kuwa hajapata maparachichi kwa zaidi ya wiki na hata sokoni hakuna. Hali hii inasababishwa na mabadiliko ya tabianchi, hasa ukosefu wa maji unaotokana na ukame au mvua zisizotabirika, hali inayosababisha mazao kama maparachichi kushindwa kuota au kukomaa. Mazungumzo baina ya mama na Baraka yanaweka wazi jinsi mabadiliko ya hali ya hewa yanavyoathiri kilimo. Kupungua kwa uzalishaji wa chakula huathiri upatikanaji wa lishe bora kwa watu, kando na kusababisha uhaba wa vyakula sokoni. Hali hii ni mfano wa jinsi mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri usalama wa chakula na maisha ya kila siku ya jamii.

Kuyeyuka kwa Barafu Kaskazini mwa Dunia na Kuzuka kwa Moto wa Porini

Sharapov (2023) alifafanua kuwa Aktiki, eneo lenye umuhimu wa kiikolojia, linapitia mabadiliko makubwa kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kipengele cha kushangaza cha mabadiliko ya hivi karibuni katika Aktiki, hasa kuhusu barafu ya baharini ni kasi kubwa ambayo joto linaongezeka na barafu inayeyuka kwa haraka. Kupungua kwa kiwango na unene wa barafu kunaonyesha athari za ongezeko la joto duniani.

Kadiri barafu za ncha zinavyoyeyuka, jamii za asili na wanyamapori wanakabiliwa na changamoto ambazo hazijawahi kushuhudiwa. Kwa mfano:

Mama Ndege: Marafiki zangu walikuwa wanapaa kwenye anga la ustaria na waliona moto mkubwa sana msituni. Lakini kwenye sehemu zingine za dunia, marafiki zangu batabuku wameona barafu kaskazini mwa dunia inayeyuka…

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021a, 5:12- 5:28)

Kauli ya Mama Ndege inatoa uchambuzi wa kina kuhusu athari tofauti za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali ya dunia. Mama ndege anaposema kwamba marafiki zake waliona moto mkubwa msituni, anaangazia tatizo la ongezeko la joto duniani linalochangia ukame na hatimaye kusababisha moto wa porini, hali inayohatarisha maisha ya viumbe. Aidha, Mama Ndege anataja pia kuwa marafiki zake batabuku wameona barafu kaskazini inayeyuka, jambo linaloonyesha athari za ongezeko la joto katika maeneo ya baridi sana kama vile Aktiki na Antaktika. Kauli ya Mama Ndege pia inaashiria kuwa mabadiliko ya tabianchi yana madhara yasiyo na mipaka ya kijiografia, na yanaathiri sayari yote kwa namna tofauti.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Aidha, ujumbe kwenye dondoo hilo unaeleza kuwa kuyeyuka kwa barafu na moto wa porini huathiri mazingira duniani kote. Ujumbe huo unalenga kuelimisha na kuhamasisha kupitia burudani (Sabido, 2003). Barafu inayoyeyuka inakuwa wito wa dharura, ikihamasisha harakati kuelekea uendelevu na usimamizi bora wa mazingira. Vipindi vya *Ubongo Kids* vinachukua nafasi ya mapambano haya. Vipindi hivi huonyesha kubadilika kwa tamaduni na kuhama kwa aina mbalimbali za wanyama ambao wamefanikiwa katika mandhari za barafu kwa milenia. Vipindi hivi vinachunguza ustahimilivu unaohitajika ili kukabiliana na hali mpya.

Uchafuzi wa Mto, Hatari ya Magonjwa na Vifo vya Wanyama

Ogola na wenzake (2024) anaeleza kuwa kimataifa, uchafuzi wa maji ni mojawapo ya matatizo makubwa ya kimazingira kutokana na ongezeko la idadi ya watu, maendeleo ya haraka ya viwanda, shughuli duni za kilimo, uchafuzi wa mazingira, na uchafuzi wa udongo pamoja na mashapo kwa kutumia viuadudu na kemikali nyingine zinazosababishwa na shughuli za binadamu. Mito na vijito vingi nchini Kenya hupoteza ubora wa maji yanapopita katika miji na mara nyingi huchafuka kutokana na shughuli za binadamu kama utupaji ovyo wa taka na uchafuzi wa viwanda. Pia, mvua nyingi na mafuriko yaweza kuzidi uwezo wa mifumo ya usafi wa mazingira kama vile tangi ya maji taka na kuifanya kuvuja na kusafisha vichafuzi (kama mbolea na taka) kwenye mto, maziwa na baharini. Kwa mfano:

Kibena: Tunaweza tukafanya usafi lakini tukashindwa kuogolea

Koba na wenzake: Kivipi je?

Kibena: Mimi naona, maji hayawezi kuwa na rangi ya kahawia kisha tu takataka.

Koba: (Akicheka), Jameni, ebu fikirieni vizuri….

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 4:20-4:42)

Dondoo hili linaonyesha changamoto zinazotokana na uchafuzi wa mazingira, hasa vyanzo vya maji, na jinsi watoto wanavyojaribu kukabiliana na hali hiyo kwa vitendo. Kibena na wenzake wanaonyesha dhamira njema ya kulinda mazingira yao kwa kupanga kufanya usafi kila Jumamosi. Hata hivyo, Kibena anatoa tahadhari kwamba usafi usio fanywa kwa umakinifu hauwezi kutosha ikiwa chanzo halisi cha uchafuzi kama sumu ndani ya maji hakitatambuliwa. Kauli yake inaonyesha fikra za kina na uwezo wa kuchanganua matatizo kwa undani. Kwa upande mwingine, majibu ya Koba – hasa ya kucheka – yanaweza kueleza ukosefu wa uelewa wa kina au mwelekeo wa kubeza hoja za tahadhari. Mtazamo huu unatoa picha ya tofauti za mitazamo katika jamii kuhusu masuala ya mazingira: kuna wanaochukua hatua, wengine wanaoelewa kwa undani zaidi na pia wanaochukulia mambo kwa wepesi. Kauli ya Kibena kwamba “maji hayawezi kuwa na rangi ya kahawia kisha tu takataka” ina dokeza umuhimu wa kuchunguza chanzo halisi cha matatizo ya mazingira.

Pia, vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids* vinaangazia jinsi wanyama wanaoishi majini kama vile samaki hutaabika kutokana na athari za uchafuzi wa mito. Kwa mfano:

Kiduchu: Una shida gani?

Samaki: (Akikohoa) Naumwa sana. Ni haya sabuni na mapovu zote zote hizi zinanifanya nasikia vibaya!... (Anaendelea kukohoa).

Kiduchu: Nenda nyumbani ukapumzike.

Samaki: Lakini hapa ndipo nyumbani kwetu.

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 7:29- 7:45)

Kifungu hiki kinaangazia uchafuzi wa mazingira kama tishio kwa maisha ya viumbe wa majini. Samaki anayeugua kutokana na sabuni na mapovu anawakilisha madhara ya moja kwa moja ya tabia za kibinadamu zisizowajibika. Kauli ya samaki

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

kama "*Lakini hapa ndipo nyumbani kwetu*," inaonyesha hisia za huzuni na kukata tamaa kwa sababu hata katika mateso yake, hawezi kuondoka; maji hayo ndiyo makazi yake ya asili. Hili linaibua hisia nzito kuhusu wajibu wa binadamu kulinda mazingira kwa ajili yao na ya viumbe wengine wanaotegemea mazingira hayo kuishi. Hivyo, kipindi hiki kinalenga kuwazindua watoto na jamii kwa jumla kuhusu athari za kutotunza mazingira, ikiwajengea moyo wa uwajibikaji na huruma kwa viumbe hai.

Jinsi ya Kuzuia Mabadiliko ya Tabianchi

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fasihi huakisi uhusiano, mwingiliano na migongano kati ya binadamu na mazingira yao. Kupitia lugha yenye mvuto, fasihi huwasilisha maudhui yanayogusa maisha ya jamii. Msanii wa fasihi hutumia hali halisi inayomzunguka kama chanzo cha ubunifu wake. Fasihi hutumika kama nyenzo ya kusaidia jamii kukabiliana na changamoto za maisha, huku ikitoa maarifa ya kujielewa na mbinu za kutatua matatizo mbalimbali yanayoukumba ulimwengu kwa ujumla. Kwa mujibu wa Reuveny (2007), watu wana mitazamo tofauti kuhusu suala la uchafuzi wa mazingira: baadhi yao huchagua kuishi katika mazingira machafu bila kuchukua hatua yoyote; wengine hukubali tu hali hiyo kama changamoto ya kimazingira; na wapo pia wanaochukua jukumu la kufanya mabadiliko ili kuboresha maeneo yaliyoathiriwa.

Kupitia elimu burudani, vipindi vya *Ubongo Kids* huchochea matumizi ya njia rafiki kwa mazingira kama njia ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mfano:

Shiko: Tunaweza tukaipanda hapa

Msaidizi wa Shiko: Mamilioni ya hela ambazo…

Shiko: Hii ndio biashara sasa…

Mwanafunzi 1: Unawezaje kufanya hivyo?

Shiko: (Akielekea aliko Koba) Utakuwa mfanya biashara mmoja mzuri kijana. Ulikuwa sahihi. Tunaweza kupanda miti hapa kufunika eneo hili lote na kuongeza msitu halafu watu ulimwenguni kote watakuwa wanatulipa kwa kufanya hii kazi kwa sababu tutakuwa tunavuta kaboni inayotoka angani na kuihifadhi kwenye ardhi. Inaitwa… Inaitwaje vile?

Mwanafunzi 1: Krediti za kaboni…

(Ubongo Kids Kiswahili, 2021b, 33:12- 33:45)

Mazungumzo haya yanaangazia umuhimu wa uhifadhi wa mazingira kupitia upandaji miti. Mazungumzo haya yanadhihirisha kuwa miti inaweza kusaidia kupunguza hewa ya kaboni na hivyo kulinda mazingira. Pia, mazungumzo haya yanaonyesha jinsi uhifadhi wa mazingira unaweza kugeuzwa kuwa fursa ya kiuchumi kwa jamii. Ni jukumu la binadamu kuheshimu na kutunza dunia kama sehemu muhimu ya maisha yao. Watu wanafaa kupanda miti, kutumia nishati mbadala, na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa mazingira. Kipindi hiki kinaandaa watoto kuwa raia wanaojali mazingira, wakijenga hisia ya uwajibikaji kwa maumbile mapema.

Hatimaye, ushirikiano na uwajibikaji pia husaidia kuzuia mabdiliko ya tabianchi. Kwa mfano:

…Lazima tupambane kwa pamoja kila saa, lazima tubadilike na kuishi kwa kujali kuwa tabia nchi inabadilika…

(Ubongo Kids Kiswahili, 2023, 0:13-0:21)

Kauli hii inatilia mkazo kuhusu jukumu la kila mtu kuchukua hatua ya kulinda mazingira. Watazamaji kwenye kipindi wanaelimishwa kuwa mabadiliko ya tabianchi si suala la mtu mmoja au taasisi moja, bali ni changamoto inayokumba watu wengi. Watazamaji wanaraiwa kubadilisha mienendo yao kupitia kauli kama, ‘lazima tupambane kwa pamoja’ na ‘lazima tubadilike na kusihi kwa kujali tabianchi inabadilika’. Burudani kwenye kipindi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

hiki cha vikatuni huchochea mabadiliko ya tabia kwa njia isiyo ya kulazimisha, bali kwa kushirikisha kihisia na kielimu na kuifanya hadhira kuona kuwa kulinda mazingira ni jukumu lao la kila siku wala sio jambo la watu wa fani fulani pekee.

Afya na Usafi

Fasihi ya watoto imekuwa chombo muhimu katika kuhamasisha maadili ya kiafya na usafi miongoni mwa watoto (Ngugi, 2017). Maudhui haya huandikwa kwa lugha rahisi na yenye mvuto, ili kuafikiana na uwezo wa ufahamu wa watoto na kuwahamasisha kwa njia ya burudani. Naye Mwilaria na wenzake (2024) wanaeleza kuwa fasihi ya Kiswahili ya watoto imekuwa na mchango mkubwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya afya kama vile magonjwa na umuhimu wa usafi. Kwa sababu hiyo, kazi nyingi za fasihi ya watoto zimeandikwa zikilenga kuangazia masuala haya. Hii ni kutokana na ukweli kwamba afya ni nguzo muhimu katika ustawi wa jamii na katika kufanikisha maendeleo endelevu.

Usafi wa Mazingira

Kwa mujibu wa Wesonga na wenzake (2020), uchafuzi wa mazingira ni jambo lililoenea kila pahali. Ni suala linaloendelea kuzungumziwa katika nyanya mbalimbali ikiwemo katika fasihi. Hata hivyo, Wesonga na wenzake wanaonya kuwa suala la uhifadhi wa mazingira huenda likawa suala ngumu iwapo binadamu hawatajitolea kuikabili vilivyo. Nchini Kenya na sehemu nyingi za dunia inakabiliwa na changamoto kama vile ukataji miti ovyo, uchafuzi wa mazingira, uhaba wa maji na usimamizi hafifu wa taka (*National Environment Management Authority*, 2021). Ukuaji wa haraka wa miji na viwanda umesababisha ongezeko la uchafuzi wa hewa na maji, hasa katika miji kama Nairobi na Mombasa. Aidha, Kenya imechukua hatua kukabiliana na changamoto hizi, zikiwemo kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki na kutekeleza sera za kuboresha usimamizi wa taka. Hata hivyo, eneo taka haramu na utekelezaji hafifu wa sheria za mazingira bado ni vizingiti vikuu. Uchafuzi unaotokana na maji machafu na taka za viwandani umesababisha kuenea kwa bakteria sugu kwa viuavijasumu, hali inayofanya magonjwa kama vile kifua kikuu na homa ya matumbo kuwa magumu kutibu.

Usafi wa mazingingira hupeperushwa kupitia njia ya burudani kwa kutumia kauli za kwenye vipindi hivi vya vikatuni. Kwa mfano:

…Usafi wa mazingira. Shirikiana nasi kuzuia maradhi, Okota takataka. Saidia jamii…

(Ubongo Kids Kiswahili, 2017a, 0:30- 0:38)

Dondoo hili linalenga kuhimiza usafi wa mazingira na ushirikiano wa kijamii katika kuzuia magonjwa. Usafi wa mazingira ni suala nyeti katika jamii ya kisasa, hususan mijini na maeneo yenye msongamano wa watu (*National Environment Management Authority*, 2021). Matumizi ya burudani kuwasilisha ujumbe mzito kwa hadhira huondoa ukavu wa ujumbe wa moja kwa moja kwa kutumia kauli kama vile "Safisha mazingira'' na “shirikiana nasi”. Pia, kauli hii huongeza ushawishi kwa kuwa watu wanapoburudika, wako tayari kupokea maarifa.

Kauli iliyonukuliwa imewekwa katika muktadha wa vikatuni, ambavyo vina sifa ya kuvutia, kuchekesha, na kufundisha bila kuchosha. Vipindi hivi vinavyotumia sauti na picha hufanikiwa kuvutia umakini wa watoto na kuwa chombo bora cha kuwafundisha wanafunzi wadogo kuhusu usafi. Kwa mujibu wa Sharma (2003), vipindi vya televisheni huwaburudisha watazamaji kando na kuwafunza. Watoto wanaweza kujifunza kuhusu usafi wa mazingira kupitia hadithi za kuburudisha na kugusa hisia. Burudani huwasaidia kuelewa umuhimu wa kudumisha usafi wa mazingira kwa njia ya kufurahisha na isiyosahaulika. Kwa kuwasilisha usafi kwa njia ya kufurahisha na inayoeleweka, watoto wana uwezo wa kukubali tabia hizi kama sehemu ya mifumo yao ya kila siku. Aidha, vipindi hivi vinakuza hisia za uwajibikaji wa kimazingira na kuwasaidia watoto kutambua

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

kwamba hata vitendo vidogo, kama vile kuweka taka kwenye takataka au kudumisha chumba chao kikiwa safi, vinaweza kuwa na athari chanya kwa jamii kubwa na kwa dunia nzima.

Umuhimu wa Lishe Bora na Mazoezi

Okowa (2024) aliweka wazi kuwa Kenya inakabiliwa na mzigo wa wa ujalivu na utapiamlo. Upungufu wa virutubisho pamoja na magonjwa yasiyo ya kuambukiza yanayotokana na lishe vinaongezeka kwa pamoja. Takriban Wakenya milioni 23 walikabiliwa na utapiamlo na mwaka wa 2022, asilimia kumi na nane ya watoto wachanga chini ya umri wa miaka mitano walikuwa wamekudumaa, huku asimilia kumi wakiwa na uzito mdogo kuliko inavyostahili (Okowa, 2024). Kitovu cha janga hili ni mfumo wa chakula uliogawanyika nchini Kenya, unaokumbana na changamoto za uzalishaji, minyororo ya ugavi isiyo na ufanisi, na athari za uharibifu zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Ngugi (2017) alibainisha kwamba maisha ya kisasa yameleta changamoto na matarajio mapya yanayomhusu mwanadamu hasa ya afya. Hali hii ya mabadiliko katika jamii imesababisha umuhimu wa kuzingatia masuala ya afya katika muktadha wa elimu ili kumwezesha mtoto kuelewa kwa kina mazingira yanayomzunguka.

Katika muktadha wa lishe bora na mazoezi, vipindi vya *Ubongo Kids* vinatumika kama njia ya burudani na elimu vinavyowasilisha maudhui ya afya kwa watoto kwa njia rahisi na ya kuvutia. Kauli kama *"Wanga hutupa nguvu mwilini. Twahitaji kuishi vyema"* (Ubongo Kids Kiswahili, 2025, 0:40: 0:47) zinaonyesha umuhimu wa vyakula vya nishati katika shughuli za kila siku, hasa kwa watoto wanaohitaji nguvu kwa michezo na masomo. Aidha, tamko *"Protini hujenga mwili na kurekebisha seli zetu"* (Ubongo Kids Kiswahili, 2025, 1:37: 1:45) linaeleza mchango wa protini katika ukuaji wa mwili, jambo linalofungamana na umuhimu wa mazoezi yanayohitaji misuli imara. Vilevile, "*Mboga na matunda zinatulinda na magonjwa. Hutujengea kinga na kutulinda" (*Ubongo Kids Kiswahili, 2025, 2:32- 2:40) inasisitiza uhusiano kati ya lishe bora na kinga ya mwili, ambayo ni muhimu kwa mtoto anayejihusisha na mazoezi ya kila siku. Matunda huwa chanzo kikubwa cha vitamin na madini na kupunguza hatari ya magonjwa mwilini. Ingawa sukari na chumvi vinatumika kuongeza ladha, watazamaji wanafunzwa kutozitumia kwa wingi kwani huenda zikaathiri mwili.

Ikoro (2022) anadhihirisha kuwa vikatuni huweza kushawishi umma kwa kupunguza ugumu wa kuelewa mambo ya kijamii ili kufanikisha mabadiliko, pale panapohitajika. Kwa kuangazia vyakula hivi kwa mtazamo chanya, vipindi hivi kwenye *Ubongo Kids* vinawahamasisha watoto kuanza kuthamini lishe bora tangu utotoni. Hali hii inaafikikiana na mawazo ya Sabido (2003) anayesema kuwa watu huweza kujifunza kupitia elimu burudani. Watoto hujifunza suala la lishe bora huku wakifurahia vipindi vya kuburudisha.

Ulinzi wa Watoto

Kwa mujibu wa Ngugi (2017), watoto wana haki ya kutunzwa, kulishwa, kuvishwa kusomeshwa, kutodhulumiwa na hata kupewa nafasi ya kushiriki michezo na wenzao. Hata hivyo, Gitonga (2022) alieleza kuwa nchini Kenya kwa ujumla, kumekwa na ukosefu wa utii wa masharti ya haki za mtoto, hasa yanayohusu ulinzi wa maslahi bora ya watoto. Ingawa Kenya imepiga hatua katika kulinda haki za watoto—hasa baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Watoto ya mwaka 2022—bado kuna changamoto kama vile watoto wengi kukumbana na ukatili mtandaoni, itikadi kali, kuondolewa kwa watoto katika taasisi za malezi na tatizo la ulinzi wa watoto wa jinsia mbili. Vilevile, watoto wengi wanadhulumiwa kingono ila hawana ujasiri wa kuripoti visa hivi.

Katika vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*, watoto wanafunzwa kuhusu haki zao za kutoruhusu kudhulumiwa. Kwa mfano:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

…usinishike nywele bila ridhaa, usinishike ngozi bila ridhaa...

(Ubongo Kids Kiswahili, 2018b,19:00-19:09)

Kutokana na dondo hili, watoto wanaelimishwa kuhusu haki zao za kimwili na umuhimu wa ridhaa. Kauli hio inasisitiza kwamba kila mtoto ana haki ya kuwa na udhibiti kamili juu ya mwili wake. Kuguswa, kushikwa au kushughulikiwa kwa namna yoyote ile inayohusiana na mwili wake kunapaswa kufanyika kwa hiari na kwa idhini yake. Kauli hio ina uhusiano wa karibu na suala la unyanyasaji wa kingono ambalo ni suala linaloibuka na linaloendelea nchini Kenya. Thaker (2025) anafafanua kuwa umri wa wastani wa wasichana kufanya ngono kwa mara ya kwanza ni miaka 11.7 (chini ya miaka 12), na karibu asilimia 100 ya matukio hayo hayakuwa kwa hiari wala kutakikana. Mara nyingi matendo hayo husababishwa kwa kulazimishwa na wanaume wakubwa kwa umri. Wakati mwingine, watoto hawa hawajui kuwa wanaweza kusema "*hapana*" au hawakujua jinsi ya kusema "*hapana*," mara nyingi kutokana na utamaduni wa kijamii wa kumtii mtu mzima bila kujali matokeo ya vitendo au maamuzi. Maichuhie (2025) naye anaripoti kuwa watoto wa kiume pia wananyanyaswa kingono kwani mwaka wa 2020, serikali ilibaini kuwa wanaume zaidi ya mia mbili walidhulumiwa kingono jijini Nairobi, 121 wakiwa chini ya 11 huku 87 wakiwa kati ya mika 12 na 17.

Kwa mujibu wa Wangamati na wenzake (2019), unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto nchini Kenya unaonekana kuchangiwa na masuala ya maendeleo pamoja na ukosefu wa usawa wa kiuchumi, kijamii na kijinsia. Mambo haya ni pamoja na shinikizo la rika, matumizi ya dawa za kulevya na vileo, uyatima, umaskini, ushawishi wa mitandao ya kijamii, utamaduni wa ukimya kuhusu masuala ya ngono, na tofauti kubwa za kijinsia kwani Thaker (2025) anabainisha kuwa msichana mmoja kati ya watatu wa umri wa miaka 19 nchini Kenya ni mjamzito au tayari ana mtoto. Pia, kuna uwezekano wa mara tatu zaidi wa wanaume nchini Kenya kujiua ikilinganishwa na wanawake.

Aidha, vipindi kuhusu haki za watoto huweka msingi wa kuwasaidia watoto kuelewa kuwa wanapaswa kujihisi salama, kuheshimiwa, na kuwa na uwezo wa kukataa jambo lolote linalowahusu kimwili. Kauli ya: "*...usinishike bila ridhaa…"* pia inalenga kulinda watoto dhidi ya aina mbalimbali za unyanyasaji wa kimwili na kingono. Kwa kuwaelekeza kwamba hawapaswi kushikwa nywele au ngozi bila ridhaa yao, watoto wanajengewa uwezo wa kutambua vitendo visivyofaa na kujua kuwa si kila mguso unakubalika, hata kama inafanywa na mtu mzima au anayewajua.

Elimu

Elimu inaendelea kubadilika duniani kote kadri changamoto mpya zinavyojitokeza. Gitau na wenzake (2023) wanaeleza kuwa elimu shuleni inapaswa kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na changamoto za kisasa kwa kuwapa maarifa, ujuzi, na maadili yenye maana. Schleicher (2018) anaongeza kuwa mfumo wa elimu unapaswa kulingana na mabadiliko ya kijamii ili kuwajenga wanafunzi kuwa wabunifu na wenye uwezo wa kutumia elimu yao katika maisha halisi. Ndiyo maana mtaala wa umilisi nchini Kenya ulianzishwa mwaka wa 2017 ili kuwasaidia wanafunzi kutumia maarifa yao kutatua matatizo ya kila siku kwa ubunifu. Mtaala huo umeweka mkazo katika masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (Wataka na wenzake., 2021). Hata hivyo, changamoto kama uhaba wa walimu na miundombinu duni bado zipo.

Televisheni, kama chombo cha mawasiliano, imekuwa daraja muhimu kati ya elimu na maisha halisi (Özer na Avcı, 2015). Vipindi kama vya *Ubongo Kids* hutoa elimu ya kisayansi kwa njia ya kuvutia na rahisi kueleweka. Vipindi hivyo vinaonyesha kwa vitendo umilisi wa teknolojia, hisabati, na sayansi**.**

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Ondimu (2018) anasema kuwa katika umilisi wa teknolojia, upungufu wa maarifa ya kidijitali miongoni mwa walimu ni changamoto. Lakini teknolojia ikitumika vizuri, huboresha matokeo ya ufundishaji (Owala, 2021). Vipindi vya *Ubongo Kids* huziba pengo hili kwa kuhusisha teknolojia katika mafunzo. Kwa mfano:

Ngendere: …sasa naambiwa redio hio inapatikana mia moja na mbili na nusu FM. Inaitwa redio Mikuge. Sasa nimekuja kujaribu katika redio yangu hii, nakuta mtindo ulioandikwa ni tofauti. Hapo ndio wakanichanganya kabisa. Njoo muone wenyewe…

Kibena: Nishagundua, unajua nini Kiduchu, Ngendere hajui desimali na ndio maana ameshindwa kujua kabisa kama namba alilotajiwa ipo katika redio...Sikiliza Ngendere ili usitusumbue tena siku nyingine, ngoja tukuelekeze kitu.

Kiduchu: Mwambie faster Kibena tukacheze mpira

Kibena: Wewe unakumbuka kuhusu sehemu?

Ngendere: Yeah, nakumbuka

Kibena: Sasa kama unakumbuka leo nataka nikuambie kwamba kuna mtindo mwingine wa kuandika namba na mtindo huu unaitwa desimali. Katika desimali, tunaandika namba, nukta, namba. Hii ina maana kwamba namba kabla ya nukta ni kitu kamili…

(Ubongo Kids Kiswahili, 2014, 5:47–7:12)

Dondoo hili linaonyesha jinsi kutokuelewa dhana za kihisabati, kama desimali, kunavyoathiri matumizi ya teknolojia. Vipindi hivyo husaidia watoto kuelewa maudhui ya kitaaluma kwa kuyahusisha na maisha yao ya kila siku. Sharma (2023) anaeleza kuwa ujumbe wa kijamii kwenye vipindi vya hivi huunganishwa na mazungumzo ili kuvifanya vivutie na kuelimisha

Katika umilisi wa hisabati, changamoto kubwa ni kuboresha uelewa wa dhana miongoni mwa wanafunzi (Mwangi na wenzake, 2024; Mong'ina, 2025). Hisabati kwa muda mrefu imekuwa changamoto kwa wanafunzi wengi nchini Kenya, na maendeleo ya hivi karibuni yanaonyesha kuwa bado ni suala muhimu (Mong'ina, 2025). Uanzishaji wa mtaala wa umilisi umeibua mjadala kuhusu iwapo hisabati inapaswa kuendelea kuwa ya lazima katika shule za upili ya juu. Aidha, Brown (2017) alisisitiza kuwa vipindi kwenye televisheni vinaweza kutumika kuelimisha kando na burudani. Vipindi vya *Ubongo Kids* hufundisha hisabati kupitia burudani, kwa mfano:

…Tisa jumlisha tisa ni kumi na nane. Naandika tisa hapa, nabeba moja…

(Ubongo Kids Kiswahili, 2020, 0:23–0:40)

Dondoo hili linaonyesha ujifunzaji wa dhana ya mjumuisho, inayosaidia wanafunzi kutumia hisabati katika maisha ya kila siku kama kupanga bajeti au muda. Mtaala wa Umilisi unalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi hawajifunzi kwa kukariri tu, bali wanapata uelewa wa kweli unaowawezesha kutumia hisabati kwa ufanisi katika mazingira halisi ya maisha yao ya kila siku.

Kwa upande mwingine, ufundishaji wa masomo ya sayansi nchini Kenya ni suala ibuka, hasa kwa kuzingatia vipengele vinavyohusiana na mafunzo ya walimu, upatikanaji wa rasilimali, na marekebisho ya mtaala. Ufundishaji wa sayansi hukumbwa na changamoto kama uhaba wa walimu, matumizi duni ya rasilimali za kufundishia sayansi, pamoja na hitaji la maendeleo ya kitaaluma kwa walimu (Odhiambo, 2024). Licha ya changamoto, vipindi kama vya *Ubongo Kids* husaidia kukuza uelewa wa kisayansi. Kwa mfano:

…Lakini tukiwa huku duniani, tunalizunguka jua, tunalizunguka wakati wote…Kwa Kiingereza tunasema orbiting...Hatulizunguki kwa haraka hivyo, inachukua mwaka mmoja kwa dunia kumaliza mzunguko mmoja...

(Ubongo Kids Kiswahili, 2017b, 3:01–3:56)

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Katika muktadha wa mtaala wa umilisi, maelezo haya kwenye dondoo kuhusu mzunguko wa dunia na mwezi yanatoa fursa muhimu ya kujifunza sayansi kwa njia inayohusiana moja kwa moja na maisha halisi. Dondoo hilo linaonyesha jinsi vipindi vya *Ubongo Kids* vinavyorahisisha dhana za kiastronomia kama mzunguko wa dunia, ikihusisha mafunzo hayo na maisha halisi kama misimu na shughuli za kibinadamu. Hivyo, vipindi hivi huchangia kukuza fikra za kisayansi na uwezo wa wanafunzi kuelewa ulimwengu kwa kina.

Usalama Mtandaoni

Weru na wenzake (2017) wanadai kuwa mtandao umejaa maudhui na shughuli zinazowaburudisha na kuwaelimisha watoto. Mamilioni ya watoto wanatumia mtandao na kubadilishana barua pepe na ujumbe mfupi na kuvinjari mtandao mpana wa dunia. Masuala yanayohusu usalama wa mitandao, ulaghai mtandaoni na ulinzi wa watoto yameongezeka kwa kiasi kikubwa. Nao Humphrey na wenzake (2023) wanaweka wazi kuwa watoto wanakabiliwa na ongezeko la hatari mtandaoni, jambo linalochochea juhudi za kuboresha uelewa wa kidijitali na elimu ya usalama mtandaoni. Vijana huripoti kwamba wakati mwingine hukumbana matukio hasi mtandaoni yanayowafanya wajihisi kutokuwa salama, kama vile kuonyeshwa maudhui ya kuhuzunisha na ugumu wa kuondoa yaliyomo mtandaoni. Maudhui kama picha na video zinazolenga mtu binafsi au kikundi kutokana na jinsia, rangi au utambulisho wa kijinsia, au ambazo ni za kikatili au za kuchukiza, yanachukuliwa kuwa na matatizo makubwa. Kadri matumizi ya mtandao kwa watoto na vijana yanavyozidi kuongezeka, ndivyo pia wasiwasi kuhusu usalama wao mtandaoni unavyozidi kuongezeka.

Katika muktadha wa mawasiliano ya kisasa, watoto huwekwa wazi kwa dhana ya intaneti kwa kuelekezwa kuhusu matumizi yake yenye manufaa hasa kwenye vipindi vya vikatuni vya *Ubongo Kids*. Kwa mfano:

…Chagua nini cha kuweka ambacho hakina madhara, usiweke chochote, kisicho na heshima. Unachoposti chaweza umiza hisia za wengine…Usiweke chochote usichooweza kufanya hadharani, utawajibika na utendacho mtandaoni. Nyayo za kidijitali, kila mahali unaziacha…

(Ubongo Kids Kiswahili 2019, 0:47- 1:14)

Kutokana na dondoo hili, watazamaji huelimishwa na kuonywa kuwa wanapaswa kumakinika kwa kile ambacho wanafanya, kuandika na kupakia mtandaoni kwani kila kitu kinaacha nyayo ya kidijitali mtandaoni. Nyayo hizi humwezesha mtu mwingine kufuatilia na kujua mtu mwingine kiurahisi. Tofauti na nyayo zingine, inakuwa vigumu kufuta nyayo za mtandaoni. Kile ambacho mtu anachapisha mtandaoni kina faida na hasara na hivyo basi watu wanapaswa kuchagua ni nini wanafaa kuweka mtandaoni. Pia, watazamaji wanahimizwa kutochapisha chochote mtandaoni wasichoweza kufanya hadharani au kinachoweza kuuumiza hisia za wengine. Intaneti ni kama uwanja wa dunia nzima kwani kile mtu anachapisha mtandaoni inaweza kutazamwa na wazazi, walimu na marafiki zetu. Hatimaye, watazamaji wanajifunza umuhimu wa kutumia intaneti kwa uwajibikaji. Pia, watazamaji wanajifunza kuhusu madhara ya kushiriki taarifa binafsi na umuhimu wa kudumisha faragha mtandaoni.

HITIMISHO

Kwa ujumla, lengo la utafiti huu lilikuwa ni kujadili masuala ibuka katika vikatuni vya *Ubongo Kids*. Utafiti ulibainisha kuwa vipindi hivi hutumia burudani kuwaelimisha watoto kuhusu changamoto zinazoathiri maisha yao, kama vile mabadiliko ya tabianchi na usalama mtandaoni. Pia utafiti huu ulibainisha kuwa vipindi katika *Ubongo Kids* huwasilisha masuala kuhusu umuhimu wa lishe bora na mazoezi, elimu, usafi wa mazingira na ulinzi wa watoto. Masuala haya hujitokeza katika vipindi mbalimbali katika *Ubongo Kids*. Hatimaye, utafiti huu ulisisitiza kuwa vipindi vya vikatuni vya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Ubongo Kids huburudisha watazamaji, hukuza maarifa, huhamasisha na kuwaelimisha watoto.

MAREJELEO

Boyd, J. (2015). *Racializing in comic books: An examination of marvel comics the punisher* (2004) St. Mary's University, Halifax, Nova Scotia.

Brown, W. (2017). Entertainment-Education. Communication. https://doi.org/10.1093/obo/97 80199756841-0180

Callus, P. (2018). The rise of Kenyan political animation: tactics of subversion.

Eko, L. (2010). The Art of Criticism: How African cartoons discursively constructed African media realities in the post-cold war era, *Critical African Studies*, 2:4, 65-91, DOI: 10.1080/20407211.2010.10530758

Gitau, A. W., Wamalwa, E. W., & Kevogo, S. A. (2023). Tathmini ya mbinu za ufundishaji wa masuala mtambuko katika mtaala wa umilisi: Mfano wa shule za msingi nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(2), 73–83. https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1645

Gitonga, S. (2020, August 18). *Which TV channel are your children watching the most? - Business Today Kenya*. Business Today Kenya. https://businesstoday.co.ke/which-tv-channel-are-your-children-watching-the-most/

Greg, G. (2004). *Ecocriticism.*London and New York: Routledge.

Humphry, J., Boichak, O., & Hutchinson, J. (2023). Emerging online safety issues: co-creating social media with young people-research report. *Emerging Online Safety Issues-Co-creating social media education with young people-Research Report*

Ikoro, O. S. (2022). Cartoon as a veritable vehicle for societal change. *maiden edition*, 118-136.

Imaizumi, S. K. (2009). *Children's television: Trends around the World*. https://www.nhk.or.jp/bunken/english/reports/pdf/05_no4_07.pdf

IPCC. (2013). Climate change 2013: The physical science basis. Contribution of Working Group 1 to the Fifth Assessment Report of the New York, NY, USA: Cambridge University Press. Available: http://www.climatechange2013.org/images/uploads/WGS_AR5_SPM_Bronchure.pdf

Karani, J. (2021). Edutainment in children's television programming: A content analysis of 'Big Minds Childrens Programme' on KBC Channel 1 (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Kidenda, M. C. (2006). An investigation of the impact of animated cartoons on children in Nairobi (Doctoral dissertation).

Maichuhie, K. (2025, April 20). *Silent tears: How Kenya's boys are battling a sexual violence crisis*. Daily Nation; Nation. https://nation.africa/kenya/news/gender/silent-tears-how-kenya-s-boys-are-battling-a-sexual-violence-crisis--5005808

Maureen, M. (2015). Masuala ibuka katika riwaya ya kisasa. *Kidagaa Kimemwozea* na *Mhanga Nafsi Yangu* (Tasnifu). Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Mong'ina, M. (2025, February 18). *Solving Kenya's math crisis: How innovation, mindset, and policy can solve Kenya's numeracy crisis*. StorySpotlight. https://storyspotlight.co.ke/solving-kenyas-math-crisis-how-innovation-mindset-and-policy-can-solve-kenyas-numeracy-crisis

Motswaledi, T. R. (2022). Political cartoons: Agenda-setters of climate change. *Journal for*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Creativity, Innovation and Social Entrepreneurship (JCISE), *6*(2), 74-84

Mwangi, I., Ndanu, C., & Awino, J. (2024). The extent to which teachers' Application of Problem-Solving Teaching Approaches Influences Learners' acquisition of creativity and imagination skills in the implementation of CBC in private primary schools in Embu West Sub-County, Kenya. *Journal of Popular Education in Africa*, *8*(9), 50-71.

Mwilaria, R., Kobia, J. and Musyimi, D. (2024). Sitiari za kiafya katika fasihi ya Kiswahili ya watoto: Mfano wa Nimefufuka, Pendo Katika Shari ya Sitaki Iwe Siri. *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp.504–513. doi:https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2351.

Naeem, M., Ozuem, W., Howell, K., & Ranfagni, S. (2024). Demystification and actualisation of data saturation in qualitative research through thematic analysis. *International Journal of Qualitative Methods*, *23*(23). https://doi.org/10.1177/16094069241229777

Nanda, V. (2011). *Climate change and environmental ethics*. New Jersey: Transaction Publishers.

National Environment Management Authority. (2021). *State of Environment Report 2019-2021: Summary for Policy Makers*. Retrieved from https://www.nema.go.ke/images/Docs/EIA_1920- 1929/SoE%202019- 2021%20SUMMARY%20FOR%20POLICY%20MAKERS%20.pdf

Neil, C. (2012). Comics, linguistics and visual language: The past and future of a field in: F. Bramlett (Ed) *Linguistics of the Study of Comics*, New York: Palgrave Mcmillan.

Ngugi, P. (2017). Usawiri wa masuala ibuka katika fasihi ya watoto: Mifano kutoka Kenya. *Mulika Journal, 35(1).*

Njeru, M.K., Kobia, J.M. and Musyimi, D.M. (2022). Usawiri wa motifu za kimazingira katika tamthilia ya Kiswahili: Tathmini ya Majira ya Utasa (Arege, 2015). *East African Journal of Swahili Studies*, 5(1), pp.151–160. doi:https://doi.org/10.37284/jammk.5.1.699.

Njogu, K & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Odhiambo, J. (2024, October 28). *Solutions to the shortage of science teachers in Kenya*. Business Daily. https://www.businessdailyafrica.com/bd/opinion-analysis/columnists/solutions-to-the-shortage-of-science-teachers-in-kenya-4804116

Ogola, J. O., Olale, K., Mogwasi, R., & Mainya, O. (2024). Organochlorine pesticide residues in water and sediments in river Kibos-Nyamasaria in Kisumu County: An inlet river of Lake Victoria, Kenya. *Scientific African*, *23*(3), e02094–e02094. https://doi.org/10.1016/j.sciaf.2024.e02094

Okowa, R. (2024). *From fast food to fresh: How to shift Kenya's eating habits to nutritious, farm-to- fork foods*. GAIN. https://www.gainhealth.org/media/news/fast-food-fresh-how-shift-kenyas-eating-habits-nutritious-farm-fork-foods

Ondimu, S. M. (2018). *Teachers' preparedness for the implementation of the Competece Based Curriculum in Private Pre-Schools in Dagoretti Sub-County Nairobi City County*. [Masters' thesis, University of Nairobi]. Nairobi.

Opunde, S., Wandera, S. & Nabea, W. (2018). Uchunguzi wa masuala ya kijinsia katika nyimbo za Daudi Kabaka na John Amutabi Nzenze. *Coretrain Journal of Humanities, Social Sciences and Education.* 1. 315-322.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Orodho, A. (2003). *Essentials of education and social science research methods*, Nairobi's: Masola Publisher.

Owala, O. R. (2021). Success and challenges of implementation of the competence-based curriculum in Kenya.

Özer, D. and Avcı, İ.B. (2015). Cartoons as educational tools and the presentation of cultural differences via cartoons. *Procedia - Social and Behavioral Sciences*, 191, pp.418–423. doi:https://doi.org/10.1016/j.sbspro.2015.04.355.

Prithviraj, M. M., Alam, M. R., & Devi, N. (2024). The cartoon character syndrome: Navigating the impact on childhood development in the digital age. *Indian Journal of Psychiatry*, *66*(5), 463– 465. https://doi.org/10.4103/indianjpsychiatry.indianjpsychiatry_201_24

Reuveny, R. (2007). Climate Change-induced migration and violent conflict. Political geography26, 656-67.

Sabido, M. (2003). The origins of entertainment-education. In *Entertainment-education and social change* (pp. 83-96). Routledge.

Schleicher, A. (2018). Educating learners for their future not our past. *ECNU Review of Education*. 1(1), 58-75. doi:10.30926/ecnuroe2018010104

Sharapov, D. (2023). Arctic ice changes and global warming. *E3S Web of Conferences*, *460*(4), 08014. https://doi.org/10.1051/e3sconf/202346008014

Sharma, N. (2023). Entertainment-Education behind the scenes: Case studies for theory and practice. *International journal of communication (Mtandaoni)*, *17*, 6417-6420.

Simala, I. (2016). "Fasihi ibuka ya Kiswahili: Hali na mustakabali wake". Katika *Kiswahili na Utandawazi*. L.C Mwita (Ed.). Nairobi: Twaweza Communications

Thaker, R. (2025, May 22). *This is what Kenya should do to end rising cases of child sexual abuse*. The Standard; Standard Digital. https://www.standardmedia.co.ke/opinion/article/2001519703/this-is-what-kenya-should-do-to-end-rising-cases-of-child-sexual-abuse

Toromade, S., Aanuoluwa, D., Kupa, N. E., & Ignatius, T. (2024). Reviewing the impact of climate change on global food security: Challenges and solutions. *International Journal of Applied Research in Social Sciences*, *6*(7), 1403– 1416. https://doi.org/10.51594/ijarss.v6i7.1300

Ubongo (2024). *Home - Ubongo Learning African Children's Media & Edutainment*. [Online] Ubongo. Available at: https://www.ubongo.org/.

Ubongo Kids Kiswahili. (2014, March 29). *Ubongo Kids Webisode 11 - Redio ya Desimali*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=lmwLGl0X3co

Ubongo Kids Kiswahili. (2017a, October 2). *Usafi wa Mazingira | Ubongo Kids Sing-along | African Educational Cartoons*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=p9LFzRwAwhQ

Ubongo Kids Kiswahili. (2017b, October 20). *Ubongo Kids Webisode 43 - Mfumo wa jua | Katuni za Kiswahili*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=nx NR7a98hiQ

Ubongo Kids Kiswahili. (2018, October 31). *Webisode 54: Ridhaa Yangu! | Ubongo Kids + European Union | Katuni za Elimu*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=6Fp_tVDEqKo

Ubongo Kids Kiswahili. (2019, July 24). *Unaweka Nini Mtandaoni?! | Imba na Ubongo Kids |*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.3.3948

Katuni za Kiswahili. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=NQAUq-AE1B4

Ubongo Kids Kiswahili. (2020, March 23). *Jifunze jinsi ya kujumlisha desimali! | Darasani na Ubongo Kids | Katuni za Kiswahili*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=YfSjH2emZE4

Ubongo Kids Kiswahili. (2021a, August 25). *Tufanye nini kuzuiia mabadiliko ya tabia ya nchi? | Darasani na Ubongo Kids | Katuni za Kiswahili*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=-_vruscPjjE

Ubongo Kids Kiswahili. (2021b, November 26). *Mabadiliko ya tabia ya nchi! | Jifunze kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira na Ubongo Kids!* YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=53PbgK_BEHE

Ubongo Kids Kiswahili. (2023, October 18). *Mabadiliko ya tabia ya nchi!* YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=z1QniceeFAg

Ubongo Kids Kiswahili. (2025, February 13). *Umuhimu wa Lishe Bora | Lishe ni Muhimu | Ubongo Kids #nutrition*. YouTube. https://www.youtube.com/watch?v=8Hk3hen0xQE

Weru, T., Sevilla, J., Olukuru, J., Mutegi, L. and Mberi, T. (2017). *Cyber-smart children, cyber-safe teenagers: Enhancing internet safety for children*. [online] IEEE Xplore. doi:https://doi.org/10.23919/ISTAFRICA.2017.8102292.

Vasquez, A. (1983). *Art and society in essays in Marxist aesthetics*. New York: Monthly Review Press.

Wangamati, C. K., Yegon, G., Sundby, J., & Prince, R. J. (2019). Sexualised violence against children: a review of laws and policies in Kenya. *Sexual and Reproductive Health Matters, 27*(1), 16– 28. https://doi.org/10.1080/26410397.2019.1586815

Wataka, N. J., Choge, S. C., & Manasseh, L. M. (2021). Tathmini linganishi kati ya mtalaa wa 8.4.4 na wa umilisi wa 2.6.6.3 katika ufundishaji wa fonimu za kiswahili katika kiwango cha chekechea. *East African Journal of Swahili Studies, 3*(1), 1–9. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.267

Wesonga, E.L., Ambuyo, B.A. and Chimerah, R. (2020). Nafasi ya fasihi katika kuwasilisha masuala ya mazingira kupitia riwaya Teule Tikitimaji (2013) na Msimu wa Vipepeo (2006) za K. W. Wamitila. *East African Journal of Swahili Studies, 2*(2), pp.54–64. doi:https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.192.

Wizara ya Elimu. (2002). Ministry of Education and Technology: Primary school education syllabus. Volume 1. Nairobi: Ministry of Education

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.